Kukua Katika Kristo

“Kwa kifo chake msalabani Yesu alizishinda nguvu za uovu. Yeye aliyewatiisha pepo wachafu wakati wa huduma yake hapa duniani amezivunja nguvu zao na kuthibitisha mwisho wao ni uangamivu usioepukika. Ushindi wa Yesu utupatia ushindi dhidi ya nguvu za uovu ambazo bado zinatafuta kututawala, tunapo tembea naye kwa amani, fyraha, na uhakika wa upendo wake.Sasa Roho Mtakatifu anakaa ndani yetu na kututia nguvu. Tukidumu kujikabidhi kwa Yesu kama Bwana na mwokozi wa maisha yetu tunawekwa huru kutoka katika mzigo wa matendo yetu yaliyopita. Hatuishi tena gizani, katika hofu ya nguvu za uovu, ujinga, na katika kukosa maana kwa namna ya maisha yetu ya awali,. Katika uhuru huu mpya ndani ya kristo, tumeitwa kukua katika kufanana na tabia yake, tukiongea naye kila siku katika sala, na kujilisha neno lake kikamilifu, tukikusanyika pamoja kwa ajili ya ibada, na kushiriki katika utume wa kanisa. Tukijitoa katika kuwahudumia kwa upendo wale wanaotuzunguka na kuwashuhudia wokovu wake, kuwepo kwake nasi daima kwa njia ya Roho hugeuza kila wasaa na kazi kuwa uzoefu wa kiroho.” (Zab.1:1, 2; 23:4;77:11, 12; Kol.1:13, 14; 2:6, 14, 15; Luk.10:17-20; Efe. 5:19, 20; 6:12-18; 1Thes.5:23; 2Pet.2:9; 3:18; 2Kor.3:17, 18; Filp.3:7-14; 1Thes.5:16-18; Mt.20:25-28; Yoh.20:21; Gal.5:22-25; Rum.8:38, 39; 1Yoh. 4:4; Ebr.10:25)

Kuzaliwa huleta furaha. Mbegu ikiota humfurahisha mkulima, mtoto akizaliwa hufurahisha wazazi hata kumfanya mama asahau uchungu aliokuwa nao. Taifa likizaliwa, nako huleta furaha na watu waweza kuandamana wakipunga mikono, bendera au matawi kushangilia kuanza kwa taifa. Furaha zote zilizotajwa, zitayeyuka ikiwa mtoto hatakua, miche haitaendelea kukua au taifa kuvia. Kukua ni jambo muhimu kwa mambo ya kiroho pia.

Maisha Huanza na Kifo

Kanuni ya msingi kuhusiana na maisha ya kikristo ni kwamba maisha huanza na kifo, naam matukio mawili ya kifo. Kwanza, kifo cha Yesu msalabani kimewezesha maisha mapya kuanza (Kol. 1:13, 14), maisha huru kwa hukumu ya dhambi (Rum. 8:1) na huru kutokana na adhabu ya kifo (Rum. 6:23) na kuleta suluhisho na Mungu. Hivyo maisha mapya kuanza. Pili, kifo cha nafsi ambacho hutufanya tuweze kupokea maisha ya Kristo.

Kifo cha Yesu. Msalaba ndiyo nguzo ya mpango wa Mungu wa wokovu. Pasipo msalaba, Shetani asingeshindwa. Damu ya Yesu hutusafisha na udhalimu wote (1Yoh. 1:7). Vurugu zote alizotenda Shetani ilikuwa kumchokoza Yesu asitekeleze kile ambacho Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa. Kwa kukubali kufa, Yesu alimvua Shetani enzi na mamlaka (Wafil. 2:15). Yule ambaye alitaka kufanana naye aliye juu (Isa.14:14) sasa ameabika kwa wale ambao wamehama kwenye nguvu za giza na kuingia kwenye ufalme wa Mwana wa Mungu (Kol. 1:13). Hivyo msalaba wa Kristo: -

Ni njia ambayo msamaha wa dhambi unawezeshwa (Kol. 2:13). Ni uthibitisho kwamba ulimwengu umepatanishwa (2Kor. 2:19). Ni ushahidi wa kuwezekana maisha ya ushindi dhidi ya miili na nia zetu (Rum. 6:12) na kufanywa wana na binti za Mungu (Rum. 8:14). Ni uthibitisho kwamba dunia hii ya dhambi, siku moja itasafishwa (Uf. 21:1).

Katika kila hatua ya ngazi ya wokovu na ushindi, tunaona ushahidi wa kutimia unabii wa Yesu kwamba alimwona Shetani akianguka kutoka mbinguni kama umeme (Luk. 10:18). Damu ya Yesu ilimwangika kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi (Mt. 26:28).

Gharama ya kuokoa kutoka dhambini ni kubwa mno yaani pasipo damu ya Yesu, hakuna ondoleo (1Pet. 1:19). Tulipokuwa hatuna nguvu, Yesu alikufa kwa ajili yetu (Rum. 5:6, 8). Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo alivyotuondolea dhambi. (Zab. 103:12). Ni kifo cha Yesu, ndicho kinatupa kuonja uzuri wa maisha mapya (Efe. 2: 14-16).

Kifo cha Nafsi. Jambo la pili muhimu katika upya wa maisha ya kikristo ni kuifia nafsi. Muumini huwa amesulubiwa pamoja na Kristo…si yeye aliye hai bali Kristo (Wagal. 2:20-21). Kanuni ya Yesu juu ya maisha mapya, ni kwamba chembe ya ngano lazima ife, ndipo izae (Yoh. 12:24). Lazima liwepo badiliko kamilifu (2Kor.5:17). Kielelezo cha ubatizo ni kwamba tunakufa, tunazikwa na kufufuka katika upya wa uzima (Rum.6:3,4). Kipo kitu kinachotokea mtu anapomkubali Yesu kama Bwana na Mwokozi wake. Woga huondoka badala yake mtu anakuwa jasiri, kutokuamini kunapisha imani, wivu na kijicho hupisha upendo. Ubinafsi hutoweka na kupisha kujaliana. Dhambi hukosa nafasi kwenye maisha ya mtu. Utu wa kale huwa umevuliwa kabisa (Kol. 3:9,10). Yesu alisisitiza "mtu awaye yote atakaye kunifuata, na ajikane mwenyewe ajitwike msalaba wake anifutate(Mt. 16:24). Hivyo wito wetu ni kuufuata msalaba, ili hekima yetu isiwe ya wanadamu bali katika nguvu za Mungu (1Kor. 2:5).

Kuishi Maisha Mapya. Jambo la tatu muhimu katika maisha ya kikristo ni kuishi maisha mapya. Kuko kutokuelewa kwa maisha ya kikristo kwamba wokovu umetolewa bure na wengine huishia hapo. Ni kweli tumekombolewa kwa damu kwa wingi wa rehema zake (Efe.1:7) na kwamba tumeokolewa kwa neema, mtu yeyote asije akajisifu (Efe. 2:8, 9). Ndiyo wokovu ni bure, lakini neema ya bure, haimaniishi neema isiyo na gharama. Neema isiyo na gharama ingelazimu kuhubiri msamaha pasipo kutubu, ubatizo pasipo nidhamu ya kanisa au kushiriki meza ya Bwana pasipo kuungama. Neema isiyo na gharama haina ufuasi/uanafunzi, haina msalaba, haina Yesu aishiye ndani yetu! Paulo anasema alikuwa alivyo kwa kuwa neema ilifanya kazi ndani yake (1Kor. 15:10). Hivyo anawasihi wakristo wasipokee neema bure (2Kor. 6:1).

Viashiria vya Kukua Katika Kristo

1. Maisha ya Kiroho. Yesu alimwambia Nikodemo, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa roho hatauona ufalme wa Mungu (Yoh. 3:5). Pasipo Roho, maisha ya kikristo hayawezekani. Ni Roho wa kweli (Yoh.14:17) atuongozaye katika kweli (Yoh.16:13), ahakikishiye dhambi, haki na hukumu (Yoh.16:7,8). Roho hutufanya sisi kuwa wana wa Mungu (Rum. 8:14) na kwa Roho Kristo hukaa nasi (1Yoh.3:24). Roho akikaa ndani yetu, twabadilika, tunakuwa viumbe vipya, vilivyopatanishwa na Mungu, tuliokombolewa na kuwekwa huru kwa kutengwa na dhambi ili tukue katika haki (Rum. 8:1-16). Tutaakisi taswira ya Yesu kutoka utukufu hadi utukufu (2Kor.3:17, 18). Roho anatufanya warithi pamoja na Kristo kwa mema hata kwa kuteswa pamoja naye (Rum.8:17). Tunalindwa kwenye dunia hii kwa ombi la Yesu kwamba pamoja na kwamba tuko ulimwenguni, sisi siyo wa ulimwengu (Wafil. 3:20). Maisha yenye nguvu ya roho yatakataa matendo ya mwili (Gal. 5:19-21) na kujawa na tunda la Roho (Gal. 5:22, 23)

2. ***Maisha ya upendo na umoja.*** Maisha ya kikristo hukomesha kutengwa na Mungu kulikoletwa na dhambi (Isa.59:1, 2). Mungu ametupatanisha kwa njia ya Kristo (2Kor. 5:18). Katika kukombolewa, huzaliwa jumuia ya waliokombolewa ambao Yesu aliomba wawe na umoja (Yoh. 17:20, 21). Mifarakano iliyoleta kubaguana yalifishwa kwa kupokea maisha mapya (Efe. 2:11-16). Amri ya kipekee katika Injili ya upendo, amri mpya (Yoh. 13:34)

hutawala. Ni amri hiyo ambayo torati yote na manabii husimamia (Mt. 22:36-40). Tunapompenda Mungu, upendano wetu sisi kwa sisi huongezeka.

3. ***Maisha ya Kujifunza Biblia*****.** Chakula ni muhimu kwa ajili ya kukua. Mwanadamu hataishi kwa mkate peke yake isipokuwa kwa neno la Mungu (Mt.4:4). Mtunga Zaburi alisema, moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutenda dhambi (Zab.119:12). Neno lina nguvu kutuwezesha kutambua mema na mabaya (Ebr. 4:12) na hivyo tutayatumia maneno yenye pumzi ya Mungu kuonyana na kutiana moyo (2Tim. 3:16, 17).

4. ***Maisha ya Maombi*****.** Mungu huzungumza nasi kupitia nasi kwa njia ya neno lake. Sisi huwa tunamwendea kwa njia ya maombi. Tunahimizwa kuomba kwa ajili yetu na kwa ajili ya watakatifu (Efe. 6:18). Twaweza kukosea kwa kuonyesha kiburi cha sala kama Farisayo (Luk. 18:11) lakini sala ni jambo la unyenyekevu. Mifano ya maombi ni mingi katika Biblia. Yesu (Mk. 1:35) Daudi (Zab. 88:1,2) na Danieli (Dan. 6:10). Maombi huwa hayana kikomo (1Thes.5:17).

5. ***Maisha yenye Matunda*****.** Kwa matunda yao, Yesu alisema, mtawatambua (Mt. 7:20). Ni kweli twaokolewa kwa neema wala siyo matashi yetu (Efe. 2;8-10 Yoh. 3:16). Lakini hatuokolewi ili tutende yanayotupendeza ila tutende yanayompendeza Mungu. Matendo mema ni matokeo ya imani itendayo kazi kwa kuwa yasipokuwapo, imani imekufa (Yak. 2:17). Yesu anapozungumzia mahusiano yake na Baba yake anasema amezitii amri za Baba yake (Yoh. 15:10, 31) na anatazamia nasi tutakaa ndani yake (Yoh. 15:4) na tutampenda, hata kumtii (Yoh.14:15).

6. ***Maisha ya Mapambano ya Kiroho.*** Maisha ya kikristo siyo rahisi wala mepesi. Tuko kwenye vita halisi ya hatari. Hatupambani juu ya mwili na nyama bali nguvu na mamlaka ya giza (Efe.6:12, 13). Kwenye vita hii, malaika wa giza hutunyemelea kutupinga kama vile malaika wa nuru wanavyotulinda (Zab. 34:7, 91:11, 12, Mdo. 5:19, 20, Ebr.1:14, 12:22). Biblia husema shetani na malaika zake wanakasirikia Kanisa (Uf. 12:17), na kama simba angurumaye, huzunguka akitafuta mtu ammeze (1Pet.8, 9). Maisha ya mkristo yamejaa mitego na ndiyo maana Paulo anatumia maneno magumu “simama” “vaeni silaha!”(Efe.6:12, 13). Mungu hajatuacha peke yetu kwa kuwa ametupatia ushindi katika Kristo (1Kor.15:57). Hivyo twapaswa kudumu katika vita tukiwa tumevaa silaha na kuomba (Efe. 6:13-18).

7. Maisha ya Kuabudu, Kushuhudia na Matumaini. Kukua kikristo hakutokei kwenye utupu, kwahitajika waumini wenye imani moja kuimarika na jamii isiyomwamini Yesu ili kuimarisha imani. Baada ya Yesu kupaa, kanisa la mitume lilishiriki pamoja ibada, ushirika, kushuhudia na kujifunza maandiko (Mdo. 2:42-47, 5:41, 42, 6:7). Hivyo mtume alishauri tuendelee kukusanyika kwa ibada (Ebr. 10:24, 25). Kukua kikristo kunahitajika katika huduma (Mt.20:25-28). Kama Baba alivyomtuma Yesu, nasi tumetumwa (Yoh.20:21). Maisha ya kukua ni yenye kushuhudia daima (Mdo. 1:8). Tunakaza mwendo kwa ili kufikia mede katika Kristo (Wafil. 3:12-14). Mungu hututakasa, hutuhifadhi bila lawama hata wakati wa kuja kwake Yesu. (1Thes. 5:23).